## SEHEMU YA 4 YASHERIA

### Usajili wa Wadau

Usajili wa wadau unafanyika kwa mujibu wa kifungu na 16(5)()(b) na (c) ambacho kinampa Msajili wa Bodi ya Maziwa madaraka ya kuweka na kutunza orodha ya wadau,

Kifungu cha 17(1) kinato amri ya kusajiliwa kwa mtu yeyote ayeshughulikia maziwa,

Kifungu cha 18 na 19 kinaipa Bodi uwezo wa kukataa kumsjili mtu asiyetimiza masharti.
Usajili utafanywa na msajili wa Bodi au wakaguzi watakaoteuliwa na Bodi.
Leseni ya usajili unakwisha muda wake kila mwaka na itahuishwa kwa kulipia (retention)

## SEHEMU YA 5 YASHERIA

### Makosa na adhabu

Adhabu kwa Makosa ya kumzuia mfanyakazi wa Bodi ya Maziwa katika kutekeleza Sheria hii zimetajwa katika kifungu cha 24 cha Sheria hii ambazo ni:

- Kutozwa faini ya shilingi laki moja au kutumikia kifungo kisichopungua miezi 6 au kupewa adhabu zote mbili.
- Adhabu kwa Makosa ya kutofuata Sheria hii zimetajwa katika kifungu cha 25 (1-3) cha Sheria ambazo ni: kutozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kutumikia kifungo kisichopungua miezi minne au kupewa adhabu zote.

## SEHEMU YA 6 YA SHERIA

### Matumizi ya Fedha

Sheria imeanzisha mfuko wa maendeleo wa tasnia ya maziwa (Dairy Industry Development Fund) ambao umetajwa katika kifungu cha 26 (1-2) cha Sheria na utasimamiwa na Bodi ya maziwa.

Kazi za mfuko huu zimetajwa katika kifungu 27 (a-c) ambazo ni:

- Kugharimia shughuli za Bodi na Baraza la wadau
- Kusaidia katika shughuli mbalimbali za kuendeleza tasnia ya maziwa.

## SEHEMU YA 6 YA SHERIA

### Kanuni zilizoko chini ya Sheria ya maziwa ambazo tayari Waziri amezitunga ni:

- The Dairy Industry (Tanzania Dairy Board Financial and Staff) Regulations, 2007
- The Dairy Industry (Registration of Dairy Stakeholders) Regulations, 2007
- The Dairy Industry (Duties and Powers of the Dairy Inspectors and analysts) Regulations, 2007
- The Dairy Industry (Raw Milk Transportation) Regulations, 2007
- The Dairy Industry (Raw Milk grading and Minimum quality and safety Requirements) Regulations, 2007
- The Dairy Industry (Treatment and Disposal of Unfit Milk Regultions, 2007
- The Dairy *Industry ( Import and Export of Milk and Milk Products Regulation, 2012*

## MAWASILIANO;

S.L.P. 17029
Kitalu Na. 47 Kisasa
Nyumba 300
DODOMA

Simu : +255 734 312 428
Barua Pepe: barua@tdb.go.tz
Website: www.tdb.go.tz

BODI YA MAZIWA TANZANIA
TDB
TANZANIA DAIRY BOARD

# SHERIA YAMAZIWA, 2004 (SURAYA262)



# SHERIA YA MAZIWA, 2004 (SURA YA 262)

## Historia

1961–1965 shughuli za uzalishaji na usindikaji wa maziwa zilisimamiwa na Bodi za kanda. Wakati huo mashamba makubwa ya watu binafsi pamoja na viwanda vya kusindika maziwa ndiyo vilitawaliwa na wafugaji walimiliki asilimia 25–40 ya viwanda hivyo.

**1965** ilipitishwa Sheria mpya ya maziwa na Sheria hiyo iliunda Bodi ya Maziwa ya Kitaifa (national dairy Board-NDB) na Bodi hiyo ilifanya kazi mpaka mwaka1973.

**1974** iliundwa Mamlaka ya Maendeleo ya Mifugo (Livestock Development Authority - LIDA). Mamlaka hii iliunda taasisi chini yake zikiwemo Kampuni ya Mashamba ya Ng'ombe wa Maziwa (DAFCO), Kampuni ya Kusindika Maziwa (TDL), n.k. DAFCO na TDL ndizo zilisimamia tasnia ya maziwa. DAFCO ilisimamia mashamba ya ng'ombe wa maziwa na TDL ilishughulika na usindikaji wa maziwa na bidhaa zake katika viwanda vyake saba (7). Wakati kampuni hizi zinafanya kazi ndiyo wakati nchi yetu ilikuwa inazalisha aina zote za bidhaa za maziwa.

**1980** hadi mwanzoni mwa 1990 yalitokea mabadiliko ya sera za kiuchumi nchini mbayo yalisababisha kutaifisha viwanda na baadhi ya mashamba ya kufugia ng'ombe wa maziwa na hadi kufikia mwaka 1998 viwanda vyote vya kusindika maziwa nchini pamoja na baadhi ya mashamba ya ng'ombe wa maziwa vilikuwa vimetiafishwa. Na wakati huo ndipo soko la maziwa lisilo rasmi likaanza kutawala hali hii ilisbbisha tasnia ya maziwa kutoratibiwa ipasavyo kwani tsania ilikuwa haina msimamizi maalum.

**1998** wadau wa maziwa walikutana mjini Arusha na waliona kuwa ni vyema tasnia ya maziwa kuwa na msimmizi na hivyo ilimuliwa Sheria ya maziwa ya mwka 1965 Sura ya 590 mbayo kwa wakati huo ilikuwa hifanyi kazi irekebishwe ili tasnia iweze kupata msimmizi.

**2004** Sheria mpya ya Maziwa Sura ya 262 ilipitishwa na Sheria hiyo ndiyo iliyoanzisha Bodi ya maziwa Tanzania

# SEHEMU YA 2 YA SHERIA

## Baraza

Sheria imeanzisha Baraza (Annual Council ambalo limetajwa katika kifungu cha 4 cha Sheria Kifungu cha 5 cha Sheria kimetaja Wajumbe wa Baraza ambao ni kama wafuatavyo:

- Mwenyekiti ambaye huwa anateuliwa na Waziri wa maendeleo ya Mifugo na Uvuvi
- Mwakilishi 1 wa vikundi vya wadau vinavyotambuliwa kutoka kila wilaya
- Mwakilishi 1 wa vyama vya kitaifa vya wadau yaani Wazalishaji, Wasindikaji, na Walaji
- Wawakilishi wa Wizara na Mashirika yanayohusika na maziwa(Wizara ya Mendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Sheria– ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa–TAMISEMI, Mamlka ya chakula na Dawa– TFDA, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine SUA) na taasisi zisizo za kiserikali zinazojihusisha na maendeleo ya tasnia ya maziwa

## Majukumu ya Baraza

Majukumu ya Baraza yametajwa katika kifungu cha 7 (a–e) cha Sheria mbayo ni:

- Kuhamasisha maendeleo endelevu ya tasnia ya maziwa nchini
- Kupendekeza majina ya wajumbe wa Bodi kwa uteuzi wa Waziri mwenye husika na mifugo.
- Kupokea na kujadili taarifa kutoka kwenye Bodi ya Maziwa Tanzania
- Kumshauri waziri juu ya maendeleo ya sekta ya maziwa na kufanya shughuli nyingine zitakazohitjika katika kutekeleza Sheria ya maziwa.

# SEHEMU YA 3 YA SHERIA

## Bodi ya Maziwa Tanzania

Sheria imeanzisha Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) mbayo imetajwa katika kifungu cha 8 cha Sheria. Wajumbe wa Bodi wametajwa katika kifungu cha 9(1) (a–k) mbao ni:

a) Mwenyekiti anateuliwa na Waziri mwenye dhamana ya Maendeleo ya Mifugo wajumbe wake ni:
b)Wawakilishi 3 wa wazalishaji maziwa
c)Mwakilishi 1 wa wasindikaji
d)Mwakilishi 1 wa wafanyabisha wa maziwa
e)Mwakilishi 1 wa watoa huduma na pembejeo
f)Mwakilishi 1 wa walaji
g)Wajumbe wengine kutoka wizarani na asasi zinzoshughulika na maziwa
(Wizara ya Mendeleo ya mifugo na Uvuvi, Wizara ya Sheria–ofisi ya Mwanasheria mkuu, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa–TAMISEMI, Mamlaka ya Chakula na Dawa–TFDA, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine–SUA)

*Wajumbe () – (e) hupendekezwa na mkutano wa Baraza (annual Council)

## Majukumu ya Bodi

Majukumu ya Bodi yametajwa katika kifungu cha 7 (a–e) majukumu hayo ni mengi (20) lakini yamegawanywa katikamkundi 3 ambayo ni:

1. Kusimamia Sheria na kuratibu tasnia ya maziwa (Regulation)
2. Kuendeleza tasnia ya maziwa (Development)
3. Uhamasishaji na utetezi (Promotion and advoccy)

## Sekretarieti ya Bodi ya Maziwa

Utendaji wa kila siku wa shughulii za Bodi ya Maziwa unafanywa na Sekretrieti ambayo inaongozwa na:

- Msajili anayeteuliwa kwa kufuata kifungu cha 16(1) na ndiye Afisa Mtendaji Mkuu na pia ni katibu wa Bodi na Mkutano wa Baraza la wadau.
- Chini ya Msajili kutakuwa na watumishi wengine watakaoajiriwa kwa kufuata kifungu cha 14.